**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI – KOROGWE.**

SHULE YA SEKONDARI JOEL BENDERA,
S.L.P 40,
**KOROGWE.**
NAMBA YA SIMU: 0652 449570
0684 022407

Tarehe ………………………..

KUMB NA HKM/JBSS/JINSI/F1/ ………………………

MWANAFUNZI …………………………..
S.L.P ……………….
**KOROGWE.**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI JOEL BENDERA HALMASHAURI YA MJI KOROGWE.</u>**

Ninafuraha kukutaarifu kuwa amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo ………………….. HONGERA SANA!.

1. Shule ya Sekondari Joel Bendera ipo umbali wa kilometa 10 kaskazini/mashariki wa Halmashauri ya Mji Korogwe. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 Usiporipoti ndani ya wiki 2, mzazi wako atachukuliwa hatua kali za kisheria.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia.**
   Sare ya shule.
   - Wasichana sketi ndefu yenye Marinda ifike kwenye kifundo cha mguu (kijani kibichi) pea mbili.
   - Wavulana suruali kijani kibichi (deep green) upana chini inch 14 pea mbili.
   - Viatu vyeusi vya kamba vyenye kisigino pea mbili kwa wote.
   - Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana na mkanda wa suruali mweusi usio na chuma kikubwa.
   - Mashati meupe mikono mifupi – mawili.
   - Sweta lifanane na rangi ya sare (kijani kibichi)
   - T-sheti za shule zitapatikana shuleni.

3. **Sheria na kanuni za shule hii.**
   Shule hii inaendeshwa kwa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.
   - Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni nakusimama kwenye uwanja wa mikusanyiko.
   - Kila mwanafunzi anapaswa kuwa mtiifu na mwenye nidhamu nzuri
   - Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maadili na utapewa nakala yeke mara baada ya kuripoti shuleni.
   - Mwanafunzi atakayetoka nje ya shule bila ruhusa atafukuzwa shule.
   - Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na silaha yoyote shuleni yake mara baada ya kuripoti shuleni.
   - Mwanafunzi atakayetoka nje ya shule bila ruhusa atafukuzwa shule.
   - Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na silaha yoyote shuleni au kitu chochote chenye ncha kali.
   - Kila mwanafunzi aoneshe heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla.
   - Mahudhurio kila siku kwenye maandalio ya jioni (Preparation)
   - Kuwahi katika shughuli nyingine atakazopewa.
   - Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka iliyopo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
   - Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

- Kuvaa ware ya shule muda wote inapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Uwe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika na kamba na sio vya kuchomeka (Bajaji) na soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana viatu na soksi jozi mbili.
- Siku ya kufungua shule uje umevaa sare ya shule ya msingi ili upimwe sare za shule fundia atakuwepo shuleni siku hiyo.
- Awe na begi la madaftari (sio marbollo) madaftari makubwa 12 kalamu, penseli, ufutio, mathematics set na Dictionary ndogo (kamusi ya kiingereza Oxfoed English Disctionary).
- Hati ya utambulisho wa tabibu (Form A) Hati ya kukubali kufuata sheria za shule (Form B) na hati ya mzazi kukubali kutekeleza wajibu wake kwa mtoto akiwa shuleni (Form C) Hati hizi zimeambatanishwa na ziwe zimejazwa kabla ya mwanafunzi kuripoti shuleni. Pia baadhi ya shule zimeambatanishwa.
- Ni marufumu kusuka nywele. Nywele zinapaswa kuwa fupi na safi hata kama unavaa hijabu.

**4. Makosa yafuaatyo yatakusababishia kufukuzwa shule.**

- Wizi
- Uasherati na ushoga
- Ubakaji.
- Matumizi ya madaa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
- Kupigana au kupiga
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- Kudharau Bendera ya Taifa
- Kuona au kuolewa.
- Kupata mimba, kusababisha mimba au kutoa mimba.
- Kugoma, kuchochea, uongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni
- Utoro.

**5. MAMBO MENGINE YA MUHIMU.**

a) Medical Examination form (fomu ya vipimo vya afya) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospital ya Serikali form hii ikabidhiwe kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) **Sehemu B** Tamko la mwanafunzi maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) **Sehemu C** Tamko la mzazi kukiri na kukubaliana na sheria na kanuni mbalimbali za shule.

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.

**6. VIFAA VYA USAFI.**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Jembe jipya na mpini wake | 1 |
| ii. | Ndoo ndogo | 1 |
| iii. | Skwiza ya kudekia | 1 |
| iv. | Kwanja jipya lililonolewa | 1 |
| v. | Fagio la brashi la ndani | 1 |
| vi. | Fagio la shelewa la nje | 1 |

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU KATIKA SHULE HII.**

..........................

**NASSON E. MSEMWA**
**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI JOEL BENDERA
S L P 40-KOROGWE

## MEDICAL FORM

(To be completed by the medical respect to form I entrants).

Pupil's full name ..............................................................................................................

Age ............................................. Year ..................................... Sex ...........................

School Examination ...........................................................................................................

Urine examination ..............................................................................................................

T.B Test ..............................................................................................................................

Heating ...............................................................................................................................

Sigh ....................................................................................................................................

Abdomen ...........................................................................................................................

Spleen ................................................................................................................................

Pregnant test .......................................................................................................................

Any other abnormalities e.g physical defects chromic family diseases cts

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

I certify that the above pupil is fit until for admission into a boarding / Day Secondary School

Signature ................................................... Designation ..........................................

Station ....................................................... Date ....................................................

## SEHEMU B: TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi .........................................................nakubali kufuata sheria zote za shule bila kuvunja hata moja kwani nimesoma sheria zote zinazonihusu nikiwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Joel Bendera na endapo nitakwenda kinyume najua nitachukuliwa hatua na uongozi wa shule hivyo naahidi kuzifuata sheria zote na kupokea maelekezo yote nitakayopewa baada tu ya kuripoti shuleni. Pia naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu wa kusoma na kujifunza kwa bidii bila kupoteza muda ili kupata elimu yenye manufaa kwangu.

Sahihi ............................ Tarehe ................................

## SEHEMU C: TAMKO LA MZAZI

Mimi ................................................... Mzazi wa ........................................ aliayechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Joel Bendera nakubali kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa mtoto wangu kama nilivyoelekezwa katika fomu hii kwamba baada ya kuisoma na kuielewa vema. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote yanyaohitajika shuleni kwa wakati na nitafuatilia mahudhurio ya mwanangu shuleni na kuzuia utoro, mimi kama mzazi nitashrikiana na wazazi wenzangu katika kuinua taaluma hapa shuleni nitahudhuria vikao vyote mbalimbali vya wazazi wa shule hii na kushiriki kwenye shughuli mbalimbali zitakazonihusu kama mdau wa elimu hapa shuleni, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vikao vya wazazi na kushiriki maamuzi mbalimbali ya wazazi.

Sahihi .................................... Tarehe ......................................